**OFISI YA WAZIRI MKUU**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**MKOA WA DAR ES SALAAM NA GEITA**
**MTIHANI WA MAANDALIZI KABLA YA UPIMAJI WA UTAMILIFU ARPILI 2026**
**KIDATO CHA NNE**
**015 ELIMU YA DINI YA KIISLAMU**

## MWONGOZO WA USAHIHISHAJI

### SEHEMU A (Alama 16)

1.

| i | ii | iii | iv | v | vi | vii | viii | ix | x |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| B | C | A | E | B | D | C | D | E | A |

**@ 01 = 10**

2.

| **ORODHA A** | i | ii | iii | iv | v | vi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **ORODHA B** | G | E | H | A | C | B |

**@ 01 = 06**

### SEHEMU B (ALAMA 54)

**3. Haki za viungo vya mja**

i) Kiwiliwili
Mwanadamu anapaswa kukitendea haki kiwiliwili kwa kupata muda wa kupumzika, na hii ni miongoni mwa ibada iliyosahaulika kwa wengi katika watu.

ii) Haki ya Midomo na Ulimi.
Ni kula, kunywa na kuzungumza yaliyohalalishwa na sio yaliyoharamu. Rejea Qur'an (16:114)

iii) Haki ya Mikono na Miguu.
Ni kushika na kuendea vyote vilivyoamrishwa na kuacha vilivyokatazwa. Rejea Qur'an (25:72)

**Hoja tatu @ 03 = 09**

**4. Mahari inavyoshusha hadhi ya mwanamke**

i) Kama mahari itafanywa ndiyo bei na thamani ya mwanamke anayeolewa kwa kutozwa na wazazi, huku muolewaji anakosa uhuru wa kutoza mwenyewe.
ii) Kiasi cha mahari kinachotozwa kinamfanya mwanamke muolewaji atoze (auzike) kulingana na uzuri, ukoo, hadhi aliyonayo.
iii) Mahari ikiwa kubwa sana kiasi cha kupelekea ugumu wa kuoa kwa muoaji, hivyo hifadhi ya mwanamke itakosekana katika jamii.
iv) Mahari ikitozwa kubwa au ndogo sana, kiasi cha kupelekea mzozo, kutohurumiana na kutothaminiana baina ya wanandoa pindi ikitokea wanaachana.

**Hoja tatu @ 03 = 09**

**5. Sheria**

a) chimbuko la sheria zinazotungwa na watu.
Zimetungwa na binaadamu kwa kutumia vipawa vya akili, elimu, mila, desturi, uzoefu, mazingira na matashi ya nafsi zao. **Alama 01**

b) Udhaifu sheria zinazotungwa na watu.
- i Mwanaadamu ana ujuzi wa mambo machache sana juu ya ulimwengu na yale yanayomzunguka. Rejea Qur'an (17:85)
- ii Mwanaadamu anaathiriwa sana na matashi ya ubinafsi, uchoyo, upendeleo, chuki, n.k.
- iii Binaadamu wametofautiana mno katika fikra, uoni, vipawa, uzoefu (mazoea).
- iv Mwanaadamu pia anaathiriwa sana na mabadiliko ya kimazingira na zama (nyakati).

**Hoja nne @ 02 = 08**

**6. Vitimbi vya Wayahudi Madinah**
- i) Walishirikiana na wanafiki katika kuwatia wasi wasi waislamu walipobadilishiwa Qibla kutoka Jerusalemu na kuelekea Al-Kaaba, Makkah.
- ii) Walitangaza kuwa Mtume (Sallallahu alayhi Wasallam) ni mtume wa uongo.
- iii) Waliifanyia Qur'an stihizai (mzaha). Rejea Qur'an (2:245), (3:181).
- iv) Wamjaribu Mtume (Sallallahu alayhi Wasallam) kwa kumuuliza maswali ya kubabaisha yasiyo na majibu ya dhahiri, kama vile:
- v) Kuwavunja moyo na kuwadhalilisha waislamu.
- vi) Walishirikiana na Wanafiki kwa njama za kutaka kumuua Mtume (Sallallahu alayhi Wasallam) na kuuhilikisha Uislamu.
- vii) Walivunja na kusaliti mikataba ya amani waliowekeana na Mtume (Sallallahu alayhi Wasallam).
- viii) Walichochea fitina baina ya Answar kwa kuwakumbushia ugomvi wao wa zamani baina ya Aus na Khazraj. Rejea Qur'an (3:100-101).

**Hoja sita @** $01\frac{1}{2} = 09$

**7. Ulazima wa kuwepo kwa siku ya mwisho**
- i) Wale waliofanya wema hapa duniani walipwe ujira na fadhila zao inavyostahiki. Rejea Qur'an (55:60).
- ii) Wale waliodhulumu haki za watu hapa duniani warudishe haki hizo kwa wenyewe mbele ya Hakimu wa Mahakimu. Rejea Qur'an (95:8).
- iii) Wale wababe waliofanya uovu uliokithiri hapa duniani bila kuadhibiwa wapate adhabu inayostahiki, wahukumiwe kwa mujibu wa makosa yao. Rejea Qur'an (1:4).
- iv) Watu waulizwe kwa vipi walitumia neema na vipaji mbali mbali walivyotunukiwa katika kuliendea lengo la kuumbwa kwao. Rejea Qur'an (102:8).
- v) Wabainike ni akina nani walifuata dini au njia sahihi ya maisha, waislamu au makafiri. Rejea Qur'an (16:38-39), (39:46).

**Hoja tatu @ 03 = 09**

8. **Mawazo Tofauti Kuhusiana na Uchaguzi wa Abubakar (Radhwiyallahu Anhu)**

i) Wapo wasemao uchaguzi ule ulifanyika katika mazingira ya kuchanganyikiwa, hivyo uongozi wa Kiislamu hauwezi kuchaguliwa kwa namna kama hii. *Pamoja na kuwa mkutano wa Ansar haukuwa rasmi, lakini kuchaguliwa Abubakar (Radhwiyallahu Anhu) kuliwafiki, kwa kuzingatia dokezo za Mtume (Sallallahu Alayhi Wasallam), ishara zitokanazo na Qur'an na aliyokuja kuyafanya Abubakar (Radhwiyallahu Anhu) wakati wa uongozi wake, ambayo yalidhihirisha usahihi wa chaguo la mkutano wa Thaqifa Bani Saidah.*

ii) Wapo wanaosema kuwa kutokuwepo kwa watu wa nyumba ya Mtume (Ahlul- Bayt) katika mkutano ule, kunabatilisha zoezi zima la uchaguzi wa Khalifa wa kwanza, Hii ni kutokana na usia unaodaiwa kuachwa na Mtume (Sallallahu Alayhi Wasallam) kwa "Ahlul-Bayt" muda mfupi kabla ya kutawafu kwake, Kwa hivyo Ali (Radhwiyallahu Anhu) ndiye aliyestahiki nafasi hiyo, na warithi baada yake ni wanawe na wajukuu wake. Hivyo Ukhalifa wa Abubakar, Umar na Uthman (Radhwiyallahu Anhum) ni batili kwa kuwa hao si katika Ahlul Bayt. *Msimamo huu si sahihi kwani Uislamu ni dini ya Allah, na si ya ukoo, kabila au Taifa fulani, na kwa kuwa hakuna aya katika Qur'an inayomwamrisha Mtume (Sallallahu Alayhi Wasallam) kurithisha dhima ya uongozi baada yake kwa watu wa nyumbani kwake (Ahlul-Bayt), basi jukumu la uongozi wa ummah limeachwa mikononi mwa waumini wenyewe. Kiongozi atachaguliwa kwa kuzingatia sifa stahiki tu.*

**Hoja mbili @** $04\frac{1}{2} = 09$

**SEHEMU C (Alama 30)**

9. **Qur'an si mashairi ya Mtume (Sallallahu Alayhi Wasallam) kwa sababu zifuatazo;**

i) Ujumbe wa Qur'an unatofautiana sana na ule wa mashairi kimvuto na taathira kama mshairi mashuhuri Labiib Ibn Rabiah alikiri hilo.
ii) Utaratibu wa uandishi wa ushairi ni tofauti kabisa na namna Qur-an ilivyoteremshwa na kuandika. Mfano uwepo wa vina na mizani ili shairi liweze kuimbika, ikibidi hata kanuni za sarufi ziwekwe pembeni ili shairi liimbike nk. Hii haipatikani kabisa katika Qur-an.
iii) Historia inashuhudia kuwa Qur-an si mashairi. Rejea tukio la mshairi Labiib bin Rabiia na Shairi Lake.
iv) Historia inaonesha kuwa Mtume (Sallallahu Alayhi Wasallam) hakuwahi kuwa mshairi.
v) Qur-an yenye inajieleza kuwa ni maneno kutoka kwa Allah (69:43)
vi) Qur-an yenyewe inapinga kuwa ni mashairi ya mtume (69:41).
vii) Kukosolewa kwa Mtume (Sallallahu Alayhi Wasallam) ndani ya Qur-an.

| | |
|---|---|
| **Hoja tano @** | **$02^1/_2$** |
| **Utangulizi** | **$01^1/_2$** |
| **Hitimisho** | **01** |
| **Jumla** | **15** |

10. Matendo ya Ibada ya Hijjah yanavyomuandaa mja kufikia lengo la ibada hiyo.

i) **Maandalizi na Safari ya Hijjah**
Ni lazima muislamu kabla ya kwenda Hijjah afanye maandalizi ikiwa ni pamoja na kuzidisha ucha-Mungu, kuandaa gharama, mahitaji, n.k. Hapa inaonekana kuwa mja anapaswa kutafuta rizki ya halali kwa ajili ya Ibada za Allah kama vile hii Hijjah, hii inamzoesha kujitahidi kuchuma vilivyo halali kwani vya haramu hata kama si kwa ajili ya ibada maalumu havifai, na huku ndiko kumpenda Allah kikweli kweli.

**ii) Safari ya Hijjah**
Mja anapoandaa safari hii ya Hijjah anakuwa upo tayari kuiacha familia yake na kila akipendacho kinachopatikana katika makazi yake. Hali hii inamzoesha na kumuandaa Hujaji kuwa tayari kujitoa kimali na kinafsi katika kuiendeleza dini ya Allah bila ya kuhofia magumu yoyote yatakayomtokea, kama vile hali ya hewa na mengineyo, na huku ndiko kumpenda Allah kikweli kweli.

iii) **Ihram**
Ni hali ya kuwa katika vazi rasmi na miiko kwa mwanaume mwenye kuhiji au kufanya Umrah. Hii inaonesha kuwa Waislamu wote kwa kuvaa nguo ya aina moja, bila ya kuzingatia utajiri wa mtu, rangi wala taifa. Vile vile kitendo cha kuchunga miiko ya vazi hili katika hali hii inamzoesha Hujaji kuchunga miiko mbali mbali aliyoiweka Allah katika maisha yetu ya kila siku, na huku ndiko kumpenda Allah kikweli kweli.

*iv)* **Talbiyah**
Ni kuitikia wito wa Allah (Sub haanahuu Wataala) kwa kusema yafuatayo, *"Labbayka Allahumma Labbayka. Labbayka laashariika laka labbayka. Innal-hamda Wanni'imata laka wal-mulka, laashariika laka".* Talbiya inatufunza kumuitikia Allah Mtukufu kufuata maamrisho na kuacha makatazo yake katika maisha yetu ya kila siku, ambapo huko ndiko kumpenda Allah kikweli kweli.

v) **Tawaf na Sa'i**
Ni kitendo cha kuizunguka Ka'aba mara saba kuanzia jiwe jeusi kwa mwelekeo wa kinyume na mwendo wa saa (ant clock wise) na kulibusu au kuligusa au kuashiria. Hapa mja anapata ukumbusho juu ya kumtaja Allah kwa wingi na kumtukuza daima. (Kwa kuzingatia Adhkar mbalimbali wakati wa Tawaf), ambako pia ndiko kumpenda Allah kikweli kweli.

vi) **Kupiga kambi Minaa, Mwezi 8 Dhul-Hijah, na Muzdalifah mwezi 9 kuamkia 10**
Minaa ni kitongoji kilichopo baina ya Mji wa Makkah na bonde la Arafah. Mahujaji huendelea kuleta Talbiyah ka wingi wakiwa huko, na watalala hapo (kwenye mahema) na kuondoka kesho yake (**Mwezi 8 Dhul-Hijah)** kuelekea Viwanja vya Arafa asubuhi, na jioni yake kwenda kupiga kambi Muzdalifah. Hii huwafunza mahujaji kuwa tayari kuacha majumba yao ya thamani na kulala katika mazingira yoyote yale kwa ajili ya kuitumikia Dini ya Allah. Pia huwafunza mahujaji kuwa ni wenye kufanya ibada ya kumtaja Allah katika mazingira yake yote katika maisha ya kila siku, na huku ndiko kumpenda Allah kikweli kweli.

vii) **Kusimama Arafah, Mwezi 9 Dhul-Hija.**
Arafa ni bonde lililo baina ya vilima vitatu. Mahujaji husimama humo tangu Swala ya Adhuhuri hadi Magharibi wakiwa wanaomba dua mbali mbali, kumtaja Allah kwa wingi pamoja na kusikiliza Khutba ya Kiongozi aliyekuwepo. Hii huwakumbusha mahujaji mkutano mkuu wa siku ya Kiama, ambapo hakuna atakayezingatiwa kuwa ni mbora ila amchae Allah zaidi, hivyo mja atajitahidi kufanya anayoyataka Allah ilia pate nafasi hiyo mbele ya Allah, na huku ndiko kumpenda Allah kikweli kweli.

viii) **Kutupa Mawe Minaa katika Minara Mitatu, Mwezi 10, Dhul-Hija.**
Ni kitendo kinachofanyika kuanzia Mwezi 10-13, Dhul-Hija kwa kutupa vijiwe saba kila Mnara. Zoezi hili huwafunza mahujaj kuishi kwa kumpiga vita shaytwan, kwani yeye ndiye adui mkubwa wa Dini ya Allah kutokana na ushawishi wake kwa waja wa Allah ili wasitekelaze amri za Allah. Rejea historia ya Nabii Ibrahim wakati alipokuwa akienda kumchinja mwanaye, ambako huku pia ndiko kumpenda Allah kikweli kweli.

**Hoja tano @ $02^1/_2$**
**Utangulizi $01^1/_2$**
**Hitimisho 01**
**Jumla 15**

**11. Usahihi wa Hadith za Mtume (Sallallahu Alayhi Wasallam) kwa kuzingatia matni yake.**
**Matni hiyo inatakiwa iwe na sifa zifuatazo;**

i) Isipingane na Qur'an.
ii) Isipingane na Hadith nyingine iliyothibitika kuwa ni sahihi au sahihi zaidi.
iii) Isipingsne na ukweli wa asili.
iv) Isipingane na Historia ya kweli.
v) Isiwe na maneno ya uongo ndani yake.
vi) Isimzulie Mtume kufanya jambo lililo kinyume na Uislamu.
vii) Isiahidi ujira mkubwa kwa amali ndogo wala adhabu kubwa kwa kosa dogo.

**Hoja tano @ $02^1/_2$**
**Utangulizi $01^1/_2$**
**Hitimisho 01**
**Jumla 15**